

COUNTY GOVERNMENT OF LAMU



THE COUNTY ASSEMBLY OF LAMU

THE HANSARD

Wednesday, 29th April, 2026

*The Assembly met at the
Main Chambers, at 2:30 p.m.*

[Deputy Speaker (MCA Paul Kimani Njuguna) in the Chair]

PRAYERS

Deputy Speaker (MCA Paul Kimani Njuguna): Next Order.

Clerk-at-the-Table: Questions and Statements.

QUESTIONS AND STATEMENTS

NON EXISTENCE OF FIRE STATION IN THE ENTIRE COUNTY

MCA Hope Wanjiku Mwaura (Nominated): Thank you Mr Deputy Speaker. Mr Deputy Speaker Sir, I rise pursuant to Standing Order 41(2)(C) to seek a statement from the Departmental Committee on Intergovernmental, labour and public service over the non-existence of fire station in the entire County.

Mr Deputy Speaker Sir, over the past several years our County has experienced steady population growth, urban expansion and increased economic activities. While these activities are welcome they also heighten the risk of fire related incidents and emergencies. Unfortunately, our current emergency response infrastructure remains insufficient to meet these growing demands which have placed lives, properties and livelihoods at unnecessary risk.

Mr Deputy Speaker Sir, the propose fire station aims to address these challenges comprehensively as the facility will be strategically located to ensure rapid response across key population centers and high-risk zones as witnessed recently in Mokowe where twin girls were burnt to death as a result of fire related incident.

Mr Deputy Speaker Sir, I sought to know from the Chairperson of the Intergovernmental, Labour and Public Service on the following: -

1. Why there is no single construction of fire station in the County?
2. Is there any measure put in place by the County Government to safeguard Lamu residents and their properties for fire related incidents?
3. When will the County Government provide this essential service to the County to prevent further fire related incidents?

[Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]: Any addition to that statement? If there isn't, can we get a response from the Chairperson of the relevant Departmental Committee.

MCA John Mburu Gitonga (Hongwe): Asante sana Bwana Naibu Spika. Bwana Naibu Spika naomba nipewe muda wa wiki mbili.

[Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]: Mheshimiwa Hope umeridhika na hizo wiki mbili?

MCA Hope Wanjiku Mwaura (Nominated): Bwana Naibu Spika bado sijaridhika kwa sababu jambo hili ni la dharura kwa sababu wiki iliyopita tuliweza kuwazika watoto pacha kwa sababu ya mkasa huo wa moto. Kwa hivyo ningemuomba Mwenyekiti wa kamati hiyo atuletee majibu baada ya wiki moja kwa sababu janga la moto hutokea wakati wowote.

[Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]: Mwenyekiti, jaribu kuleta majibu alhamisi ijayo ili Mheshimiwa Hope aweze kupata majibu.

Next Statement.

UKOSEFU WA VICHINJIO KATIKA ENEO LA MATONDONI

MCA Somoe Abdulrahman (Nominated): Asante sana Bwana Naibu Spika. Bwana Naibu Spika, ninachukua fursa hii kulitaarifu Bunge hili kuhusu ukosefu wa vichinjio katika masoko ya Matondoni, Wadi ya Mkomani.

Masuala yaliyobainika: -

1. Hakuna vichinjio: Wakaazi wa Matondoni hawana eneo rasmi na la usafi la kuchinjia. Hali hii inalazimisha uchinjaji usiodhibitiwa na unaleta hatari kwa afya ya wananchi, pia ni kinyume cha sharia ya udhibiti wa nyama na kanuni za afya ya umma za Kaunti.
2. Hakuna soko rasmi: Wafanyibiashara, wavuvi na wakulima wa eneo la Matondoni hufanya biashara zao mitaani. Hali hii inainyima Kaunti mapato, inaweka bidhaa za chakula katika hatari ya kuchafuka na mwisho inaleta utaratibu mbovu katika shughuli za biashara.

3. Athari za kiuchumi: Ukosefu wa miundombinu hizi zinakwamisha ukuaji wa uchumi wa eneo na unazuia uongezaji thamani kwa mifugo na samaki.

Hatua zinazohitajika kutoka kwa Waziri wa Kamati ya Utendaji ya Kaunti husika ya ukulima na mifugo:

1. Kufanya tathmini ya eneo la Matondoni ndani ya siku 30 ili kubaini ardhi inayofaa kwa ujenzi wa kichinjio cha kisasa na soko.
2. Kuwasilisha ripoti kwa Bunge hili likieleza:
 - Maeneo yaliyopendekezwa na michoro ya miundombinu hiyo.
 - Makadirio ya fedha katika mwaka wa fedha 2025/26 kwa ajili ya ujenzi.
 - Hatua za muda za kuhakikisha uchinjaji salama na biashara yenye mpangilio.
3. Kuharakisha kutangazwa rasmi kwa soko na kichinjio Matondoni ili kuhakikisha utiifu wa sharia za afya ya umma na mipango ya Kaunti.
4. Kushirikisha jamii ya Matondoni kupitia ushirikishwaji wa umma ili kuhakikisha miundombinu hiyo inakidhi mahitaji ya wananchi.

Bwana Naibu Spika Matondoni ni kituo muhimu cha uvuvi na biashara Lamu. Kuweka miundombinu hii ya msingi kutaboresha viwango vya afya, kuimarisha maisha ya wananchi na kuongeza mapato ya Kaunti.

[Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]: Mheshimiwa

Mwenyekiti wasema upewe nakala ndio uweze kufahamu zaidi ama unaweza kujibu?

MCA Suleiman Mohamed Farah (Witu): Asante sana Bwana Naibu Spika. Bwana Naibu Spika nimeielewa vizuri nakala ya Mheshimiwa Somoe, kwa hivyo naomba nipewe muda wa wiki mbili.

[Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]: Mheshimiwa Somoe umeridhika na majibu ya Mwenyekiti?

MCA Somoe Abdulrahman (Nominated): Ndio nimeridhika Bwana Naibu Spika.

Deputy Speaker (MCA Paul Kimani Njuguna): Next Order.

Clerk-at-the-Table: Motion.

Deputy Speaker (MCA Paul Kimani Njuguna): Honorable Members, there being no other business, the Assembly stands adjourned until tomorrow Thursday, 30th April 2026 at 2:30pm.

The Assembly rose at 3:50p.m.